## DIBAJI

"Kitabu hiki "Habari Njema Imekufikia" ni barua ya upendo kutoka kwa Mungu Baba kwa kila moyo unaotafuta tumaini na uzima wa kweli. Kwa lugha nyepesi na yenye nguvu ya kiroho, Dkt. George Macha anatufikisha kwenye kiini cha Injili ambacho ni Upendo wa Mungu unaookoa, unaoponya, na unaoweka huru. Hii ni zawadi halisi ya kiroho kwa kizazi chetu. Ni muhimu isomwe, ichukuliwe kwa uzito, na ipokelewe kwa upendo na moyo wa unyenyekevu."

**Mama Mataifa, Daktari Lilian Kiwone. Mrithi Mwenza Kijiweni na Roho Mtakatifu, Mkurugenzi wa kampuni ya IGGN & Royal Priest. Huduma Ya Kimataifa Pete Ya Muhuri. (Hagai 2:23)**

NAKUPENDA- ni neno linalo ogopwa kutumiwa na watu wengi hata wengine kutumia pasipo kujua maana yake halisi hadi kupelekea watu wengi kuumizwa na kutojua maana halisi ya Upendo. Ninamshukuru Mungu Baba kwa ajili ya kitabu hiki kizuri ambacho kimezidi kunionesha juu ya Upendo mkuu wa Mungu Baba kwetu ambao ndio wa kweli na mkuu kuliko wote. Ninaamini kwa kuzidi kuuelewa Upendo huu wa Mungu Baba juu yetu basi wengi tutaponywa na kuufanya 'Mwili wa Kristo' kuwa sehemu salama zaidi duniani. HAKIKA MUNGU BABA ANANIPENDA SANA!

**Evg & Dr. Prosper Tutindaga Israel, Mkurugenzi Taasisi ya Kijiweni na Roho Mtakatifu, Huduma Ya Kimataifa Pete Ya Muhuri. (Hagai 2:23)**

**SALAMU KWAKO RAFIKI…!**

Salamu kwako Rafiki! U wewe upendwaye na Mungu! U wewe ulotamanio la moyo wa Mungu! Ndio!... Si mwingine bali ni wewe kwayo mikono yako imeshika Habari Njema Hii. Salamu hii isikushangaze sana. Nimekuletea Habari Njema kuwa: Mungu Anakupenda!... Ndio, Mungu Anakupenda! Nimekueleza kuwa isikushangaze kwa kuwa Habari Njema hii huwashangaza wengi.

***"…Akaingia nyumbani kwake akasema, Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe. Naye akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu…"***

Najua kuwa unajua kila habari uliyonayo kuwa ya kweli wala si fununu au habari ya kutunga lazima iwe na Ushahidi. Kama ni habari ya ugonjwa na udhaifu lazima una ushahidi wake wa madaktari. Kama ni habari ya kukataliwa, athari za madawa ya kulevya, usaliti najua una ushahidi wake. Ndivyo ilivyo, Habari Njema hii niliyokuletea, uliyoishika, na uisomayo pia ina uthibitisho,kielelezo, na uhalisia wake, wala si habari ya dini nikuleteayo, wala tamaduni, falsafa, au hekima za duniani bali ni HABARI NJEMA ZA UPENDOWA MUNGU KWAKO!

"MUNGU ANAKUPENDA!", naamini hii sio mara ya kwanza kuisikia Habari hii Njema ya Upendo wa Mungu kwako na pengine umesikia habari nyingine kuhusu Mungu zilizo tofauti na hii niliyokuletea, labda ilikuwa kanisani, msikitini, sinagogi au sehemu nyingine za ibada, nyumbani, shule au hata katika mazungumzo ya kawaida na ndugu na rafiki.

## **YESU KRISTO**.

Je, Yesu Kristo ni nani? Je, alifanya nini? Anahusika vipi na Mungu kunipenda na kunisamehe? Najua haya ndio maswali unayojiuliza baada ya kusoma kichwa cha habari kilichokolezwa na kilichoandikwa kwa herufi kubwa.

***"…kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu…"***

Wanadamu wote ni wadhambi. Wote tumezaliwa katika asili ya dhambi wala hakuna hata mmoja awezaye kujiokoa kwa nguvu zake mwenyewe. Hivyo, katika Upendo wake Mungu kwetu, Mungu aliazimia kuifanya Mwenyewe kazi ya kutuokoa kutoka katika utawala wa shetani na dhambi.

***"…Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao…"***

## **KILA AAMINIYE, KILA AKIRIYE...**

Hii ni ZAWADI. Naiita ZAWADI kwasababu huhitaji kufanya chochote au lolote kuipata. Ni wewe kuipokea tu.! Najua nilipokuambia kuwa ni ZAWADI, na kukueleza kuwa hupaswi kufanya jambo lolote au chochote kuipokea ZAWADI hii, umejiuliza… Je, naipokea kwa namna gani? Mungu ameahidi kwamba kila aaminiye na kukiri kile alichofanya kwasababu ya Upendo wake kwetu sisi kwa njia ya Yesu Kristo yaani mateso, kifo na ufufuko wake (kwa ujumla huitwa kazi kamilifu ya Yesu Kristo ya msalabani) ataipokea zawadi hii ya msamaha wa dhambi, ukombozi na maisha mapya, MWENYEWE. maisha ya MUNGU

***"…Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu…"***